# Mikabala ya Uchanganuzi wa Hiponimia na Uainishaji Wake

*Benard Odoyo Okal*
*Chuo Kikuu cha Maseno*

**Ikisiri**

**Wataalamu mbalimbali wa Kiswahili wameshughulikia tafiti za hiponimia ya kategoria za nomino na vitenzi huku wakitoa mifano anuwai. Hata hivyo, tafiti hizo hazijadhihirisha mikabala inayoweza kutumiwa kuichanganua kama vile mkabala wa kisayansi na kiisimu. Vilevile hakuna mitindo ya uainishaji wa hiponimia ambayo imewahi kuangaziwa katika Kiswahili mbali na kutajataja tu hipanimu husika na zile hiponimu zake. Hivyo basi, makala hii imeshughulikia mikabala ya uchanganuzi wa hiponimia na uainishaji wake kwa kulenga leksimu za Kiswahili hasa za kategoria za nomino na vitenzi zilizoteuliwa kidhamirifu kutoka kamusi anuwai za Kiswahili. Makala hii imedhihirisha kuwa hiponimia inaweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia mikabala miwili: mkabala wa kisayansi na kiisimu. Aidha, uainishaji wa hiponimia za kategoria za nomino na vitenzi huweza kufanywa kwa kuzingatia mkabala wa kiisimu katika misingi sita maalum kama vile: kitambuzi, kiuamilifu, kijiografia, kitukio, kihali na kitendo.**

**Maneno Muhimu**: Hiponimia, Fahiwa, Mkabala, Taksonimia

## Utangulizi

Hiponimia ni aina maalum ya fahiwa inayoonyesha uhusiano wa kimaana baina ya leksimu ya jumla (hipanimu) inayojumuisha leksimu nyingine mahususi (hiponimu) (Lyons, 1981; Barker, 2001; Cruse, 2011; Yildirim & Yildiz, 2012; Rei & Briscoe, 2014). Kwa hivyo, hiponimia ni uhusiano unaodhihirika baina ya neno maalum na neno la jumla (TUKI, 1990). Mathalani, neno la jumla *mfugo* hujumuisha kimaana maneno mahususi kama vile *kondoo, mbuzi* na *ng'ombe*. Hiponimia za nomino huonyeshwa kwa kutumia fomyula maalum kama vile: *X* ni ***Y***, *X* ni aina ya ***Y***, *X* ni hiponimu ya ***Y***, na ***Y*** ni hipanimu ya *X* (Cruse, 1986; Hatch & Brown, 1995; Fromkin, Rodman & Hyams, 2007). Kutokana na fomyula hizi, *X* hurejelea hiponimu na ***Y*** hurejelea hipanimu. Aghalabu, fomyula hizi hutumiwa katika uchanganuzi wa hiponimia za nomino kama vile: *kondoo* ni ***mfugo***, *kondoo* ni aina ya ***mfugo***, *kondoo* ni hiponimu ya ***mfugo***, na ***mfugo*** ni hipanimu ya *kondoo*. Hata hivyo, idadi ya *X* inaweza kuwa zaidi ya moja kutegemea hiponimu zinazojumuishwa katika hipanimu husika. Hivyo basi, hiponimu mahususi kama vile *kondoo, mbuzi* na *ng'ombe* huweza kujumuishwa

moja kwa moja katika hipanimu maalum inayojulikana kama ***mfugo***. Kwa ujumla, fomyula kama hizi huweza kuonyeshwa kivielelezo kama vile:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *X* | ni***Y*** | | → | *Kondoo, mbuzi, ng'ombe* ni ***mfugo*** |
| *X* | ni | aina ya ***Y*** | → | K*ondoo, mbuzi, ng'ombe* ni aina za ***mfugo*** |
| *X* | ni | hiponimu za ***Y*** | → | K*ondoo, mbuzi, ng'ombe* ni hiponimu za ***mfugo*** |
| ***Y*** | ni | hipanimu ya *X* | → | ***Mfugo*** ni hipanimu ya *kondoo, mbuzi, ng'ombe* |

Fomyula hizi zinazotumiwa katika kategoria za nomino hazitumiwi katika udhihirishaji wa hiponimia za vitenzi. Hii ni kwa sababu vitenzi aghalabu vinahusiana kihiponimia kwa njia ya namna au jinsi bali sio kwa msingi wa aina. Hivyo basi, fomyula ya '*X* ni namna ya ***Y***' huangaziwa zaidi (Miller, 1991). Kama vile, *chemsha* ni namna ya *pika*. Katika mfano huu, leksimu *chemsha* hurejelewa kama kitenzi hiponimu (kitenzi mahususi) na *pika* ni kitenzi hipanimu (kitenzi cha jumla). Kutokana na mfano huu, hiponimu kitenzi *chemsha* basi huonyesha namna maalum ya *pika* ambacho ni kitenzi hipanimu.

Mbali na fomyula hizi, hiponimia huweza kuwasilishwa kwa kutumia mtindo wa seti ambapo alama ya epsiloni hutumiwa kuonyesha hipanimu na hiponimu zake. Alama hii ya epsiloni (∋) hutumiwa kuonyesha vile vipashio vinavyojumuishwa katika kundi maalum (Stephan, 2009; Roitman, 2011). Kimsingi, vipashio hivyo vinavyojumuishwa katika kundi maalum hudhukuriwa kama hiponimu na kundi maalum linalojumuisha hurejelewa moja kwa moja kama hipanimu. Kwa hivyo, hiponimu ni vipashio vinavyojumuishwa katika hipanimu yaani kundi maalum. Hivyo basi, tunaposema kuwa ***Y*** ∋ {*X*…}, kimsingi tunamaanisha kuwa (***Y***) ni hipanimu inayojumuisha hiponimu (*X*...). Hiponimu hizi zinaweza kuwa zaidi ya moja kutegemea mifano husika. Mathalani, ***rangi*** hujumuisha hiponimu hasa *manjano, nyekundu, samawati* na kadhalika hali inayoweza kuonyeshwa kwa mtindo wa seti kama vile:

**Rangi** ∋ {*manjano, nyekundu, samawati…*}

Fahiwa nyinginezo zinazodhihirisha uhusiano wa leksimu katika semantiki ni kama vile sinonimia (leksimu zenye maumbo tofauti kiothografia na kimatamshi lakini zenye maana linganifu), homonimia (leksimu moja ina maana zaidi ya moja zisizo na uhusiano wa kihistoria au kiasilia) na polisemia (leksimu moja ina maana zaidi ya moja ambazo zinahusiana na zina asili au historia moja). Kuna vilevile antonimia (leksimu moja ina maana inayokinzana na ya leksimu nyingine) na homofoni (leksimu husika hutamkwa kwa namna inayofanana na nyingine lakini zote zina tahajia na maana tofauti). Fahiwa nyingine ni usampuli kifani (prototype) inayoonyesha hali ya mfano bora inayodhihirika baina ya leksimu zinazounda hipanimu maalum. Mathalani, *ng'ombe* na *ngamia* ni hiponimu za *mfugo*. Hata hivyo, *ng'ombe* ni mfano bora wa *mfugo* katika jamii

nyingi kuliko *ngamia*. Kuna pia fahiwa ya meronimia inayoonyesha leksimu zinazohusiana kwa kurejelea sehemu za kitu kizima. Kama vile, *ukuta*, *sakafu* na *paa* ni *sehemu za nyumba*.

Hiponimia na meronimia aghalabu hurejelewa kama fahiwa zinazoegemea suala la ujumuishi ambapo leksimu ya jumla hujumuisha kimaana zile leksimu mahususi (Cruse, 1986). Hata hivyo, tofauti hutokea kwamba hiponimia inaposhughulikia nomino inayorejelea kitu kizima, kwa upande mwingine, meronimia hushughulikia nomino zinazorejelea sehemu za kitu kizima. Katika hiponimia, nomino zinazorejelea kitu kizima kama vile *jogoo* hujumuishwa katika nomino nyingine inayorejelea vilevile kitu kizima kama vile *kuku*. Hata hivyo, katika meronimia, nomino inayotumiwa kurejelea sehemu ya kitu hutumiwa kuonyesha uhusiano na kitu hicho kizima. Kama vile, *shingo, kichwa, kiwiliwili, mikono* na *miguu* hurejelewa moja kwa moja kama sehemu au meronimu za *mwili* ambacho ni kitu kizima.

Ingawa wataalamu wengi wameshughulikia hiponimia za leksimu nomino ya Kiswahili kama vile Gibbe (1977), Omogo (1996), Habwe na Karanja (2004), Odoyo (2006), King'ei (2010), Obuchi na Mukhwana (2010) na Mdee, Njogu na Shafi (2011), masuala ya mikabala ya uchanganuzi na uainishaji wake hayajashughulikiwa. Wataalamu hawa wameonyesha tu moja kwa moja kategoria za leksimu zinazohusiana kihiponimia kama vile nomino na vitenzi. Hata hivyo, data za kazi hizi hazijaonyesha mikabala inayoweza kutumiwa katika uchanganuzi wa hiponimia na pia jinsi ya kuainisha hiponimia kwa kutoa mifano faafu ya Kiswahili. Hivyo basi, makala hii inadhamiriwa kufafanua mikabala mikuu inayoweza kutumiwa katika uchanganuzi wa hiponimia na vilevile uainishaji wake.

Makala hii imehusisha data za hiponimia zilizokusanywa kidhamirifu kwa kurejelea kamusi mbalimbali za Kiswahili sanifu hasa kwa kulenga kategoria za nomino na vitenzi. Kategoria hizi zinahusiana kihiponimia kwa kiwango kikubwa zikilinganishwa na kategoria nyingine za lugha. Aidha, data hizi ziliteuliwa kwa kuangazia leksimu vitenzi na nomino husika zinazohusiana kihiponimia kutokana na fasili au maelezo katika kamusi husika za Kiswahili sanifu. Kama vile:

**Nikwata** *nm[*a-/wa-*]* mjusi anayeishi nje ya nyumba (Mdee *na wenzie*, 2011: 392)

Kutokana na dondoo hili, inajitokeza bayana kuwa *nikwata* ni aina ya *mjusi* hivyo basi, ***mjusi*** ni hipanimu na *nikwata* ni hiponimu yake. Fasili kama hii hudhihirika pia katika hiponimia za vitenzi. Mathalani, hiponimu *kimbia* hufasiliwa moja kwa moja kama namna ya hipanimu ***enda*** kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo:


**Kimbia** *kt*<sie>**1**. enda mbio, enda kwa kasi (Mdee *na wenzie*, 2011: 212)

Data zilizokusanywa za hiponimia za nomino na vitenzi zilichanganuliwa kwa kuzingatia mikabala na mifumo maalum ya miainisho. Ili kufaulisha dhamira ya makala hii, uwasilishaji wake umegawanya katika vitengo mbalimbali. Kuna kitengo maalum kinachoonyesha mikabala inayoweza kutumiwa kuchanganua hiponimia kama vile mkabala wa kisayansi na kiisimu. Aidha, kuna sehemu inayoshughulikia uainishaji wa hiponimia katika miainisho mikuu sita: kitambuzi, kiuamilifu, kijiografia, kitukio, kihali na kitendo. Uainishaji huu wa hiponimia aghalabu hurejelea hasa leksimu za kategoria za nomino na vitenzi vya Kiswahili.

## Mikabala ya Uchanganuzi wa Hiponimia

Wataalamu wengi wana mazoea ya kufafanua na kutoa mifano ya maneno yanayohusiana kihiponimia katika lugha husika bila kuonyesha mikabala na njia husika ya uainishaji wake. Mathalani, katika Kiswahili *mnyama* huweza kuangaziwa moja kwa moja kama hipanimu inayojumuisha hiponimu nyingi kama vile *ng'ombe, punda, kondoo, ngamia* na kadhalika bila kuonyesha mkabala maalum uliotumiwa na vilevile njia msingi ya uainishaji. Hivyo basi, mkabala maalum hufaa kuangaziwa na wataalamu ili kuonyesha ule uliotumiwa na vilevile msingi wa uainishaji wa hiponimia husika.


Baadhi ya kazi za wataalamu hudhihirisha kwamba kuna mikabala miwili ya uchanganuzi wa hiponimia kama vile mkabala wa kisayansi na wa kiisimu (Lyons 1968; Cruse 1986; Crystal 1987; Wierzbicka 1988). Mikabala hii miwili hutumiwa aghalabu kuainisha hiponimia za kategoria ya nomino kitaksonimia kamilifu au kisayansi na kitaksonimia isiyo kamilifu au kiisimu. Taksonimia hurejelewa kama njia mojawapo ya uchanganuzi msingi wa kimantiki wa hiponimia ambapo hiponimu huonyeshwa katika vielelezo tungo na kwa kurejelea sifa maalum (Hatch & Brown, 1995). Taksonimia kamilifu humaanisha ugawanyaji wa hipanimu husika katika hiponimu zake kwa kuzingatia mfumo maalum wa kibiolojia wenye mantiki. Kama vile, hipanimu *kiumbe hai* (living thing) huweza kugawika kitaksonimia kamilifu kwa kuzingatia mfumo wa kibiolojia katika hiponimu hasa *mnyama* na *mmea*. Maelezo hayo huweza kuonyeshwa katika kielelezo **1** kifuatacho:




**Kielelezo 1**: Taksonimia kamilifu kuhusu hiponimu za *kiumbe hai*

Kwa upande mwingine, taksonimia isiyo ya kisayansi au ya kiisimu huangaziwa kwa kutegemea mwelekeo wa mtu binafsi au jamiilugha husika. Kama vile, *kiumbe hai* huweza kugawika kitaksonimia ya kiisimu kwa mujibu wa

mwelekeo wa mtu binafsi au jamiilugha husika katika hiponimu *punda*, *mboga*, *samaki*, *mdudu*, *ndege* na kadhalika. Hali hii huweza kuonyeshwa katika kielelezo **2** kifuatacho:





**Kielelezo 2:** Taksonimia ya kiisimu kuhusu hiponimu za *kiumbe hai*

Ingawa taksonimia huonekana katika uchanganuzi wa hiponimia, mara nyingi haijitokezi kama mfumo halisia wakati wote kama unavyoshereheshewa katika sayansi kwa sababu ya tofauti baina ya lugha mbalimbali za kijamii (Lyons, 1968). Taksonimia huweza kuonyesha hiponimia kimatabaka kutokea tabaka la juu, kati na chini (Carter & McCarthy, 1988; Cruse, 2011; Gao & Xu, 2013) kutegemea hipanimu na hiponimu zake zinazorejelewa. Mathalani, hipanimu *samani* katika daraja la juu hujumuisha *kiti* katika daraja wastani au kati na *kiti cha jikoni* katika daraja la chini kabisa (Channell, 1994). Maelezo haya hudhihirishwa kama tunavyoonyesha katika kielelezo **3** kifuatacho:

***Samani*** → [Tabaka la juu]
*Kiti* → [Tabaka la wastani au kati]
*Kiti cha jikoni* → [Tabaka la chini]

**Kielelezo 3:** Mfumo wa kimatabaka wa hiponimu za *samani*

Mfumo kama huu wa ngazi ya kimatabaka unashereheshewa pia na Cruse (2011:168) katika hiponimu za *vyombo vya kulia* (tableware) kama tunavyoona katika kielelezo **4** kifuatacho:




**Kielelezo 4:** Mfumo wa kimatabaka wa hiponimu za *vyombo vya kulia*

Kwa mujibu wa kielelezo **4**, ngazi za kimatabaka huonekana kutokea hipanimu *vyombo vya kulia* kuja kwangazi **1** inayohusisha hiponimu kama vile

*vilia*, *krokari* na *kitambaa cha kitani* zinazogawika vilevile katika kiwango cha ngazi **2** ya hiponimu *uma, kisu* na *kijiko, kikombe, sahani* na *bilauri*, na pia *kitambaa cha meza* na *nepi*. Ngazi **3** inajumuisha *kijiko cha chai, kijiko cha meza* na *kijiko cha mchuzi* ambazo ni hiponimu za *kijiko*.

***Mkabala wa kisayansi***

Mkabala wa kisayansi hurejelea uainishaji wa leksimu za lugha unaofanywa kwa kuzingatia sifa msingi maalum za kibiolojia ambazo aghalabu hutumika kurejelea hipanimu *kiumbe hai* na hiponimu zake. *Kiumbe hai* hujumuisha kibiolojia hiponimu kama vile *mmea* na *mnyama* zinazoweza kugawika pia kitaksonimia na kimatabaka katika hiponimu nyingine mahususi. Mathalani, *mmea* hujumuisha kibiolojia *mmea uso tishu* (non vascular plant) na *mmea wenye tishu* (vascular plant) (Otto & Towle, 1977 katika Odoyo, 2006). *Mmea uso tishu* hujumuisha hiponimu kama vile *burayofaita*, *gugu maji* na *kuvu* (fungus). Sifa bainifu za kibiolojia zinazofafanua *mmea uso tishu* ni kama vile [-zailemu, -fuloemu, -majani, -mizizi, -shina] na *mmea wenye tishu* una sifa bainifu hasa [+zailemu, +fuloemu, +mizizi, +shina, +majani]. *Mmea wenye tishu* hujumuisha hiponimu zenye sifa mbalimbali kama vile: *angiospamu* [+huzaa chembekike kwenye ovari], *jimnospamu* [+hutoa mbegu zilizo wazi], na *kangaga* (fern) (Hoplant, 2002).

Kwa upande mwingine, *mnyama* hujumuisha hiponimu hasa *mnyama mwenye uti mgongo* na *mnyama aso uti mgongo* (Otto & Towle, 1977 katika Odoyo, 2006). *Mnyama mwenye uti mgongo* hujumuisha kibiolojia *amfibia, mamalia, mtambaazi, ndege* na *samaki*. Hiponimu za *mnyama mwenye uti mgongo* hufanywa kwa kuzingatia mkabala msingi wa kisayansi kwa kurejelea mifumo ya sifa bainifu za kibiolojia kama vile [+uti wa mgongo, +ufunikaji mwili na maganda au nywele, +ukakawana maungo ya mwili, +utanafusi au upumuaji, +mzunguko au mwenezo wa damu, +utoaji taka mwilini, +uundaji michomozo ya kemikali za mwili, +mishipa ya fahamu, +uzazi, +mmeng'enyo] (Otto & Towle, 1977 katika Odoyo, 2006).

*Mnyama aso uti mgongo* hujumuisha hiponimu msingi kama vile *Athropoda, Ekinodamata, Koelenterata, Molaska* na *Porifera* (Westmoreland & Esparza, 2005). Kwa mujibu wa Otto na Towle (1977) wakirejelewa na Odoyo (2006), hiponimu za *mnyama aso uti mgongo* huwa na sifa bainifu za kibiolojia kama vile *Athropoda* ina sifa bainifu za [+wasio na uti wa mgongo, +miguu inayoshikana na sehemu nyingine za mwili, +mifupa iliyo nje, +mwili uliogawika katika vijisehemu, +moyo ulio mgongoni]. Kimsingi, *Athropoda* hujumuisha hiponimu *Araknida, Kilopoda, Diplopoda, Insekta* na *Krastasia*. *Ekinodamata* hujumuisha hiponimu kama vile *kiti cha pweza* (starfish), *mwanamize* (sea urchin), *pweza mwepesi* (brittle star). *Koelenterata* hujumuisha hasa hiponimu *korali* na *mnyoo. Porifera* hurejelewa kama viumbe wasio na uti wa mgongo na huishi majini.


*Molaska* ni viumbe hai wanaoishi katika siyaki ya bahari ya maji safi kama vile *chaza/shaza* na *koa/konokono*.

Ingawa mkabala wa kisayansi wa hiponimia huelekea kufanywa kwa kuangazia sifa bainifu za kibiolojia, sifa hizi huelekea kutotumika tunapochunguza leksimu zinazorejelea sehemu za *kitu* au *viungo*, *vifaa* na *rangi*. Kimsingi, virejelewa hivi hasa sehemu za kitu, vifaa na rangi havina uhai. Hivyo basi, sifa za kibiolojia zinazoangaziwa katika mkabala wa kisayansi haziwezi kutumiwa. Mathalani, ni vigumu kuchanganua hiponimia za *rangi* kisayansi bali huweza kufanywa tu kwa mkabala wa kiisimu. Kwa hivyo tunaweza kupata hiponimu zake kama vile *nyeupe, nyeusi, nyekundu, chanikiwiti, manjano, buluu, kahawia, zambarau (purple), pinki, rangi ya chungwa* na *kijivu* zinazofafanuliwa kiisimu. Mkabala wa kiisimu hurejelea uhusiano wa leksimu kihiponimia kwa kuangazia sifa za kiisimu.

### *Mkabala wa Kiisimu*

Mkabala wa kiisimu hutegemea jinsi kirejelewa kinavyoonekana na kufafanuliwa bila kuzingatia sifa za kibiolojia bali huegemea fasili katika makala ya leksikografia ya lugha na pia ubinafsi wa mtafiti. Mathalani, *kiumbe hai* ambacho hujumuisha hiponimu kama vile *mmea* na *mnyama* kwa mujibu wa mkabala wa kisayansi huweza pia kujumuisha hiponimu kama vile *mboga* (vegetable) na *mnyama* (animal) (Crystal, 1987). Aidha, hipanimu *mnyama* hujumuisha pia *binadamu, mdudu, ndege* na *samaki* hasa tunapozingatia mkabala wa kiisimu (Crystal, 1987). Hali hii huelekea kuwa tofauti na mkabala wa kisayansi unaojumuisha hiponimu za *mnyama* kwa njia tofauti kibiolojia. Kama vile, *mnyama mwenye uti mgongo* hujumuisha *amfibia, mamalia, mtambaazi, ndege* na *samaki* na *mnyama aso uti wa mgongo* hujumuisha hiponimu *Athropoda, Ekinodamata, Koelenterata, Porifera* na *Molaska*.


Kimsingi, mkabala wa kiisimu huangazia sifa za kawaida za kiisimu kuhusu hipanimu na hiponimu husika kwa mujibu wa maelezo ya kamusini au makala nyingine za kileksikografia. Mkabala huu wa kiisimu aghalabu huhusisha mgawanyo wa kitaksonimia isiyo kamilifu au isiyo ya kisayansi. Taksonimia isiyo kamilifu hurejelea uainishaji wa leksimu husika kijamii au kiisimu ambapo hipanimu hugawika kwa mujibu wa mfumo wa kijamii, lugha husika na ubinafsi wa mtafiti. Kama vile *kiumbe hai* huweza kujumuisha kitaksonimia isiyo kamilifu hiponimu *binadamu, kondoo, mdudu, nyati* na *paka* kama tunavyoonyesha katika kielelezo **5**:




***Kielelezo* 5:** Taksonimia ya kiisimu ya hiponimu za *kiumbe-hai*


Wakati mwingine taksonimia ya kiisimu hurejelewa kama taksonimia ya kibinadamu kwa sababu hutegemea ubinafsi wa mtafiti. Hata hivyo, taksonimia ya aina hii haitokei katika ombwe tupu bali huelekea kuzingatia vilevile vigezo fulani. Mathalani, huwa na viwango vichache vya migawanyo kitaksonimia au wakati mwingine haionyeshi migawanyo, na vilevile huweza kuwa na kategoria changamano zinazohitaji kufafanuliwa zaidi (Ungerer & Schmid, 1997 katika Murphy, 2003). Uchanganuzi wa hiponimia kiisimu huelekea kurejelea muundo wa hipanimu kwa jinsi tofauti tofauti kwa mujibu wa wataalamu husika. Hivyo basi, uchanganuzi wake huonyeshwa kwa kutegemea mtafiti husika huku ukidhihirisha mianya, kutokuwa na fomyula maalum na kufuata miundo na mitindo anuwai (Ungerer & Schmid, 1997 katika Murphy, 2003). Mathalani, uchanganuzi wa *kiumbe* (creature) baina ya Cruse (1986) na Yule (1996) hudhihirisha miundo ya sampuli anuwai.

Sampuli hizi zinazotofautiana zinaweza kufafanuliwa zaidi tunapoangazia fafanuzi za Cruse na Yule. Mathalani, Cruse (1986:136) anafanya uchanganuzi wake kwa kuanzia leksimu *kiumbe* (creature) kinachorejelewa kama hipanimu na kinachoweza kugawika kitaksonimia ya kiisimu katika hiponimu maalum hasa *mnyama*, *ndege*, *samaki* na *mdudu*. Kwa upande mwingine, *mnyama* huelekea kujumuisha hiponimu *mbwa* na *ndovu*, *ndege* hujumuisha hiponimu hasa *kurumbiza* na *tai*, *samaki* hujumuisha hiponimu *chewa*, na *mdudu* hujumuisha hiponimu *chungu* na *kipepeo*. Hali hii inadhihirishwa katika kielelezo **6** kifuatacho:




**Kielelezo 6:** Taksonimia ya kiisimu ya hiponimu za *kiumbe* kwa mujibu wa Cruse (1986)


Kwa upande mwingine, Yule (1996:119) anaanzia uchanganuzi wake kutoka kwa *viumbe hai* (living things) vinavyogawika kitaksonimia ya kiisimu katika *kiumbe* na *mmea*. *Kiumbe* hugawika katika *mnyama* na *mdudu*. *Mmea* hugawika katika *mboga*, *ua* na *mti*. *Mnyama* hujumuisha *farasi*, *mbwa* na *nyoka*, na *mdudu* hujumuisha hiponimu *mende* na *chungu*. *Mboga* hugawika katika *karoti*, *ua* katika *ua la manjano* (daffodil) na *mti* katika *msonobari*. Hali hii hudhihirishwa katika kielelezo **7** kifuatacho:




**Kielelezo 7:** Taksonimia ya kiisimu ya hiponimu za *viumbe hai* kwa mujibu wa Yule (1996)

Tofauti za kimuundo tunazoweza kuona baina ya wataalamu hawa ni kwamba, Cruse (1986) anachanganua muundo wa hipanimu *kiumbe* katika hiponimu nne kama vile *mnyama, ndege, samaki* na *mdudu* huku Yule (1996) akichanganua muundo wa hipanimu *kiumbe* katika hiponimu mbili hasa *mnyama* na *mdudu*.

Tofauti nyingine za kimuundo zinazotokana na matumizi ya mkabala wa kiisimu huonekana pia katika vifaa kama vile *vyombo vya mezani vya kulia na kupakulia* (tableware) kama tunavyoona katika Cruse (1986) na Hornby (2010). Kwa mujibu wa Cruse (1986:147), hipanimu *vyombo vya kulia na kupakulia* huweza kugawika kiisimu katika *vilia* (cutlery), *vyombo vya kupakulia/vipakulizi/krokari* (crockery) na *vyombo vya kioo* (glassware). *Vilia* hujumuisha *kisu* na *kijiko, vyombo vya kupakulia* hujumuisha *sahani* na *kikombe*, na *vyombo vya kioo* hujumuisha *glasi ya mvinyo* (wine glass) na *bilauri* (tumbler). Hali hii inaonekana katika kielelezo **8** kifuatacho:




**Kielelezo 8:** Hiponimu za *vyombo vya kulia na kupakulia* kwa mujibu wa Cruse (1986)

Kwa upande mwingine, Hornby (2010) hurejelea muundo au hiponimu za *vyombo vya kulia na kupakulia* kama vile *sahani, glasi, visu* na *uma*. Tofauti

baina ya wataalamu hawa ni kwamba, Cruse (1986) anagawanya vyombo hivi kimadaraja ambapo pana *vilia, vyombo vya kupakulia* na *vyombo vya kioo* kabla ya kufikia vyombo mahususi kama vile *kisu, kijiko, sahani, kikombe, glasi ya mvinyo* na *bilauri*. Hata hivyo, Hornby (2010) anataja vyombo hivyo mahususi moja kwa moja kama vile *sahani, glasi, visu* na *uma* kutoka kwa hipanimu kuu *vyombo vya kulia na kupakulia.*

Mbali na muundo, mitindo pia huelekea kufanana au kutofautiana tunaposhughulikia suala la hiponimia kiisimu kwa mujibu wa jamii lugha husika. Mathalani, katika lugha ya Kigiriki, hiponimu hasa *daktari*, *seremala* na *mpiga filimbi* (flautist) zinazorejelea watu wasio na uhusiano wowote kitaaluma hujumuishwa kimtindo katika hipanimu moja inayojulikana kama '*demiourgos*' (Crystal, 1987). Hipanimu hii haina kisawe maalum katika Kiingereza chenye utamaduni na mtindo tofauti. Aidha, lugha ya Kiswahili pia haina kisawe maalum cha kurejelea hipanimu '*demiourgos*' inayojitokeza katika Kigiriki kwa sababu ya tofauti za kimazingira na kitamaduni. Kutokana na mfano huu, inadhihirika wazi kuwa uchanganuzi wa hiponimia kwa msingi wa mkabala wa kiisimu huweza kudhihirisha mitindo na muundo tofauti kwa mujibu wa utamaduni wa lugha husika (Lyons, 1981; Crystal, 1987).

Kwa jumla, uchanganuzi wa hiponimia kwa kutumia taksonimia ya kisayansi huonyeshwa kutokana na vigezo vya kibiolojia (Carter & McCarthy, 1988; Hatch & Brown, 1995). Hata hivyo, vigezo vya kisayansi vina nafasi finyu katika uchanganuzi wa hiponimia za virejelewa vingi katika lugha anuwai (Carter & McCarthy, 1988). Usayansi huelekea kutumiwa zaidi katika uchanganuzi wa hiponimia za *viumbe hai* na sio hiponimia za viumbe visivyo na uhai kama vile *vifaa* na *vitenzi*. Mkabala wa kiisimu hutumika mno katika uainishaji zaidi wa hiponimia za nomino na vitenzi katika lugha nyingi ulimwenguni.

## Uainishaji Kiisimu wa Hiponimia

Hiponimia za maneno ya lugha hasa ya kategoria za nomino na vitenzi huweza kuainishwa kiisimu kwa kuzingatia miainisho mikuu sita: uainishaji kitambuzi, kiuamilifu au kidhanishi, kijiografia, kitukio, kihali na kitendo (Wierzbicka, Chaffin & Herrmann, 1984 wakirejelewa na Murphy, 2003). Kila aina ya muainisho huwa na ufafanuzi wake kama tunavyoona katika sehemu zinazofuatia. Hata hivyo, uainishaji kitendo unaohusisha hiponimia za kategoria ya vitenzi hautashughulikiwa kwa kina kwa sababu tayari umeangaziwa katika kazi ya Okal, Indede na Mohochi (2016). Aidha, data za baadhi ya hiponimu za hipanimu zinazorejelewa katika sehemu zifuatazo zimeonyeshwa kwa mfumo wa safu huku upande wa kushoto ukiangazia hipanimu na upande wa kulia ukirejelea hiponimu zake.

### *Uainishaji wa hiponimia kitambuzi*

Uainishaji wa hiponimia kitambuzi aghalabu hutumiwa kutambua vitu kwa mujibu wa jinsi vinavyofanana na jinsi vinavyoonekana. Uainishaji wa aina hii huchunguza umbo la kitu fulani na kurejelea kufanana kwake na kitu kingine ili kuunda uwanda mmoja kileksika na kisemantiki. Kitambuzi, tunaweza kupata hiponimia za *kiumbe hai*. *Kiumbe hai* hutokana na dhana ya *kiumbe* inayorejelea kitu chenye uhai kama vile binadamu, mnyama, jini, ndege, samaki, wadudu, mimea, au kile kisicho na uhai kama vile miti, mimea na kadhalika (Mdee *na wenzie,* 2011; TUKI, 2013). Kutokana na maelezo haya, basi kuna fafanuzi za *kiumbe* kwa jinsi mbili: *kiumbe hai* na *kiumbe kisicho hai.* Makala hii imelenga uainishaji kitambuzi hasa wa hiponimu za *kiumbe hai* kwa kuzingatia mkabala wa kiisimu na hatimaye kutoa mifano husika. *Kiumbe kisicho hai* kimeangaziwa kikamilifu katika muainisho wa kiuamilifu. Kwa kuwa hiponimia zinazochanganuliwa kiisimu hutegemea uamuzi wa mtafiti na jamiilugha husika (Ungerer & Schimid, 1997 katika Murphy, 2003), tunaweza kurejelea baadhi ya mifano ya hiponimu za *kiumbe hai* kwa msingi wa utambuzi kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| **Kiumbe hai** | : | gegereka, mdudu, mmea, mnyama, ndege, mtambaazi, samaki. |
| *Gegereka* | : | jongoo la bahari, kaa, kamba, kasa, koa, kojokojo, nyera, pweza. |
| *Mdudu* | : | buibui, bunzi, chaki, chururu, fukusi, jongoo, kiroboto. |
| *Mmea* | : | miti, majani, nyasi, ua. |
| *Mnyama* | : | duma, farasi, ngamia. |
| *Ndege* | : | korongo, kasuku, njiwa. |
| *Nyoka* | : | bafe, chatu, firi, mamba, nondo, swila. |
| *Samaki* | : | dagaa, kambare, kamongo, ningu, perege, sangara. |

### *Uainishaji wa hiponimia kiuamilifu*

Uainishaji kiuamilifu au kidhanishi husaidia katika uchanganuzi wa hiponimia kwa kurejelea kazi zinazofanywa na vitu fulani maalum katika uwanda kileksika. Mathalani, hipanimu *samani* hujumuisha hiponimu *viti, meza* na *kabati* kwa sababu aghalabu huelekea kutumia malighafi inayolingana na pia hutumiwa ndani ya nyumba. Uainishaji kiuamilifu huweza kurejelea sio tu vifaa au vyakula pekee bali pia *viumbe hai* kwa msingi wa jamiilugha husika. Katika uainishaji kiuamilifu, *viumbe hai* hujumuisha hiponimu kama vile *atifali, binadamu, mmea, mnyama* na *ndege* zenye hiponimu anuwai:

| | | |
|---|---|---|
| **Atifali/vikembe** | : | chirika, jana, kibunju, kibwagala, kichinda, kifaranga, kifukofuko, kilebu, kiluwiluwi, kinda, |

kinyaunyau, kisungura, matumatu, mche, mtoto, mwanabata, mwanafarasi, katama, mwanapunda, ndama, njiti, shibli.

**Binadamu/mja** : fundi, jamii, mfunzi, mhalifu, mtumwa, mwendeshaji.
*Fundi* : fundibomba, fundimchundo, fundisanifu, mfinyanzi, mhandisi, mhunzi, msusi, mwashi, seremala, sonara.
*Jamii* : ali, baleghe, chemvi, maharimu, mchumba, mlezi, binamu, mwanamke, mwanamume, mseja, mshenga, mtalaka, mrithi, shemeji, wifi.
*Mfunzi* : aalimu, katekista, kungwi, mhadhiri, mwalimu.
*Mhalifu* : gaidi, mkora, mnajisi, mnyang'anyi, mviziaji, mwizi.
*Mtumwa* : abdi, kijakazi, mjoli, mtwana.
*Mwendeshaji* : dereva/dreva, rubani, nahodha.

**Mmea** : chakula, dawa, majani, mti, nyasi, ua.
*Chakula* : kiazi, kinywaji, kiungo, mboga, muhogo, nafaka, matunda.
*Dawa* : mkaumwa, mjafari, kwinini.
*Majani* : bangi, chacha, gugu, hina.
*Mti* : bobo, chakaazi, mgunga, mjakaranda.
*Nyasi* : chacha, fefe, kangaja, kwekwe, ndago, vue.
*Ua* : jaja, kakindu, kilua, mnyonyore, mrihani, nyunginyungi, shaunge.

**Mnyama** : kisakuzi, mbwawa, mfugo, ominivora, rikabu.
*Kisakuzi/Kivinjari* : punda, twiga.
*Mbwawa/Mbuai* : chui, fisi, simba.
*Mfugo* : kondoo, mbuzi, ng'ombe, ngamia.
*Ominivora/Mla yote* : panya, nguruwe, binadamu.
*Rikabu* : farasi, punda, ngamia.

**Ndege** : bata, batabukini, batamzinga, kanga, kasuku, kuku, kware, njiwa, tausi.

*Kiumbe kisicho hai* huweza kujumuisha hiponimia mbalimbali zinazoangaziwa kiuamilifu kama vile *ala za muziki, chakula, chombojikoni, chombosafari, kileo, kitilio, mtego, samani, silaha, taa* na *vazi* zilizo na hiponimu nyingine faafu kama vile:

**Ala za muziki** : ala za kupigwa, ala za kupulizwa, ala za nyuzi.
*Ala za kupigwa* : kayamba, marimba, ngoma.

| | | |
|---|---|---|
| *Ala za kupulizwa* | : | buruji, gunda, filimbi, mzumari, pembe, saksofoni, tarumbeta. |
| *Ala za nyuzi* | : | fidla, gambusi, gitaa. |
| **Chakula** | : | chakula kiowevu, chakula kigumu, chakula kiwakati. |
| *Kiowevu* | : | asali, chai, maziwa, mchuzi, sharubati, uji. |
| *Kigumu* | : | andazi, kitoweo, kiungo, lawalawa, mkate, ugali, wali. |
| *Kiwakati* | : | ambrosi, chajio, chamcha, chamshakinywa, daku, dhifa, ekarista, kiamshahamu, kisutuo, kombe, malimati, maponeo, mchapalo, pamba, pudini. |
| **Chombojikoni** | : | chomeo, chungu, chungio, karai, mwiko, samawari, sufuria, ubia, kijiko, kisu, uma, upawa, dishi, sahani, kikombe. |
| **Chombosafari** | : | chomboangani, chombomajini, chomboardhini. |
| *Chomboangani* | : | helikopta, jeti, roketi. |
| *Chombomajini* | : | boti, dau, feri, jahazi, mashua, meli, mtumbwi. |
| *Chomboardhini* | : | baisikeli, gari, kitimaguru, pikipiki, trekta, garimoshi. |
| **Kileo** | : | afyuni, amfetamini, bangi, mvinyo, pombe. |
| *Mvinyo* | : | divai, konyagi, zarambo, spiriti. |
| *Pombe* | : | akari, araka, bia, boji, buzaa, brandi, chang’aa, chibuku, dengelua, jini, kangara, komoni, manjilili, mbege, ndazi, shizi, togwa, ulanzi, uraka, wanzuki. |
| **Kitilio** | : | beseni, chupa, debe, dundu, galoni, karai, kibuyu, kikapu, kontena, kreti, mfuko, mkebe, mlizamu, mtungi, ndoo, pipa, tangi, sanduku. |
| **Mtego** | : | dema, gwato, jarife, juya, kimia, kiunda, mgono, mshipi, mwina, tando, tenga, ngavu, uwalio, vyero/uzio. |
| **Samani/fanicha** | : | kabati, kikalio, kitanda, meza. |
| *Kabati* | : | almari/saraka, dipfriza, jokofu, kabati la nguo, sefu. |
| *Kikalio* | : | deski, firasha, jamvi, kiti, mkeka. |
| *Kitanda* | : | machela, mede, mwakisu, samadari, susu/mlezi, tusi/jeneza. |
| *Meza* | : | altare, dawati, ngurunga. |

| | | |
|---|---|---|
| **Silaha** | : | bomu, bunduki, fimbo, gandalo, kombora, kisu, mkuki, mshale, mzinga, panda, shoka, teo/kombeo. |
| **Taa** | : | fanusi/kandili, karabai, kibatari, tochi, mshumaa, mwenge, seraji. |
| **Vazi** | : | kiatu, kitambaa, kofia, nguo, pambo. |
| *Kiatu* | : | buti, daluga, raba, lapa, kubadhi, mtarawanda, njuti. |
| *Kitambaa* | : | amitko, bafta, bitana, batiki, kaniki. |
| *Kofia* | : | bargashia, bereti, boshori, bulibuli, chepeo, helmeti, kidotia, kitunga, mdongea, pama, shumberere, topi. |
| *Nguo* | : | joho, kaptura, koti, nguo za ndani, shati, shuka, suruali, tandiko. |
| *Pambo* | : | bangili, bruchi, herini, jaribosi, jasi, jebu, kasabu, kikuba, kingaja, kipini, kishaufu, koa, koja, lakti, mkufu, pete. |

***Uainishaji wa hiponimia kijiografia***

Uainishaji wa hiponimia kijiografia unahusisha hiponimu za mahali kama vile X (*Kenya*, *Urusi* …) ni aina za ***Y*** (*nchi*). *Mahali* ni nafasi au eneo ambalo watu au viumbe hukaa, huishi na kufanyia shughuli nyinginezo. Mahali pa binadamu huwa na *nyumba* inayoweza kuwa na mtindo kama vile *ghorofa/orofa, msonge* (mtindo wa mviringo), *tembe* (mtindo wa nyumba fupi iliyo na paa mfuto la udongo au nyasi) na *shangama* (mtindo wa mapaa mawili). Kuna pia *bangwa* (nyumba iliyojengwa nusu na haijakamilika). Kwa jumla *mahali* panagawanywa katika: *mahali pa afya, biashara, elimu, hifadhi, kiwanda, maabadi* na *makazi*.

| | | |
|---|---|---|
| **Mahali pa afya** | : | dispensari, famasi, hospitali, kliniki, leba, maabara, pamahututi, sadaruki, sanatoria, thieta. |
| **Mahali pa biashara** | : | afisi/ofisi, baa, bengi, bucha, danguro, diro, duka, hoteli, kafeteria, kantini, kasino, kilinge, kioski, klabu, lilamu, pambajio, mauli, mesi, saluni, sinema, supamaketi. |
| **Mahali pa elimu** | : | chuo, jando, shule, taasisi. |
| **Mahali pa kuhifadhia Vitu/stoo** | : | banda, bandari, chanja, depo, ficho, forodha, ghala, kaburi, maegesho, makavazi, maktaba, makumbusho, masjala, mochari. |
| **Mahali pa kiwanda** | : | deri, flotile, gereji, joko, jokotanu, karakana, machinjioni. |

**Mahali pa maabadi**: batizo, hekalu, jamati, kaaba, kanisa, kimbilio, madhabahu, msikiti, panga, sinagogi, tabenakulo.

**Mahali pa makazi/ Makao** : ahera, arkadia, barazahi, bloku, chaa, chalia, dahalia, dimba, edeni, fuko, ganjo, hamio, jumba, kambi, kifukofuko, kijiwe, kimbilio, kiota, kirimba, kizimba, makani, makazi ya kifalme, manyata, manzili, mazalio, misheni, risavu, sasa, sega.

### *Uainishaji wa hiponimia kitukio*

Uainishaji wa hiponimia kitukio hutumiwa kuonyesha matukio yenye wahusika na malengo maalum. Uainishaji huu unatumia fomyula kama vile *X* (*kandanda, sataranji/chesi* ni aina za *Y* (*mchezo*). Kimsingi, tukio huwa na mandhari yake maalum, washiriki, lengo pamoja na vifaa vinavyotumiwa ili tukio liwe kamilifu. Tukio kama vile *mchezo* huwa na sifa bainifu kama vile ya kushinda na kushindwa, kufurahisha, hutegemea ustadi na bahati.

**Mchezo** : ajua, besiboli, biliadi, chesi, drafu, gofu, handiboli, hoki, judo, jugwe, kandanda, kriketi, masumbwi, mchezo wa kuteleza, mchezo wa kuviringisha tufe, sarakasi, mchezo wa tufe, miereka, mpira wa vikapu, mpira wa vinyoya, netiboli, raga, riadha, snuka, taekwondo, tenisi, uogeleaji, urushaji mkuki, voliboli.

### *Uainishaji wa hiponimia kihali*

Uainishaji wa hiponimia kihali hushughulikia nomino dhahania. Uainishaji wa hiponimia kihali unajumuisha hipanimu kuu hasa *malipo, sauti, ugonjwa* na *ulemavu* zinazojumuisha hiponimu mbalimbali kama vile:

**Malipo** : ada, adhabu, advansi, dia, faini, ghila, haka, hongo, honoraria, ijara, jizia, kanda, kilemba, kisasi, kotokoto, nauli, marupurupu, mrabaha, poza, rada, rubuni, thawabu, sadaka, zawadi.

**Sauti** : alamu, alhani, besi, bipu, gombea, gumio, kelele, keu, kibirikizi, kidoko, kifijo, kifoli, kigong’ondo, kimako, kwenzi, mbiu, mkoromo, mitongo, mlio wa fahali, mrindimo, mruzi, mshindo, msonyo, mteteo, mtoriro, mtutumo, mvumo, mwaliko, mwangwi, ndundu, ngurumo, nong’ono, nyende, parakacha, selo, tiktika.

| | | |
|---|---|---|
| **Ugonjwa** | : | ugonjwa wa binadamu, ugonjwa wa mmea, ugonjwa wa mnyama, ugonjwa wa ndege. |
| *Ugonjwa wa Binadamu* | : | balghamu, bombo, firangi, homa, kifaduro, kifua kikuu, mafua, ndui, tetemaji, ugonjwa wa makamasi mengi, ukunguru, busha, mgonzo, barasi, bato, chekea, chunusi, harara, kipwepwe, lengelenge, mba, ukoko, ukurutu, upele, uwawati, harisho, harisho ya damu, harisho ya amiba, kipindupindu, kobwe, mwanamimba, ngiri, riahi, chovya, halula, hijabu, jipu dogo, jipu kubwa, jongo, kikope, kipandauso, kororo, machapwi, mdudu kidole, mti, mtoki, paru, tambazi, rovu/uvimbe wa tezi, zongo, bwiko, duwazi, faliji, gangrini, kaka, kiwe, matege, mtoto wa jicho, ukoma, upofu, farangi, kisonono, pangusa, tego, tutuko, ukimwi. |
| *Ugonjwa wa Mmea* | : | bakajani, batobato, chule, chulebuni, doakahawia, doapembe, fugwe, kiitochura, kikwachu, kimatira, kinyaushi, kiozamizi, kituru, kizimwili, mkwachuro, mlandege, mnyauko bakteria, rozeti, tristeza, ubwiri, ubwirijivu, ubwiri vinyoya. |
| *Ugonjwa wa Mnyama* | : | brusilosi, chambavu, dasi, kaudriosi, kimeta, kiyungi, kuhara, mkunge, ndigana, rabizi, shuna, sotoka, vimbiwa. |
| *Ugonjwa wa Ndege* | : | gomboro, kideri, kokidiosi, mahepe, ndui. |
| **Ulemavu** | : | afkani, bubu, buge, chongo, gobwe, hanithi, huntha, kengeza, kibiongo, kibogoyo, kibwiko, kidazi, kidole cha sita mkononi, kidurango, kigugumizi, kiguru, king'ong'o, kinyonyoka, kikono, kipofu, kithembe, kiwete, kiziwi, mang'ombo, matege, mziavu, unju, zeruzeru. |

***Uainishaji wa hiponimia kitendo***

Uainishaji wa hiponimia kitendo unahusisha aghalabu hiponimia za leksimu vitenzi. Hivyo basi, huonyesha namna vitenzi vya jumla vinavyohusiana kihiponimia na vitenzi vingine mahususi. Maelezo mengi kuhusu uainishaji wa

hiponimia kitendo tayari yameshughulikiwa katika makala ya Okal *na wenzie* (2016) ambapo pana hipanimu vitenzi vya Kiswahili hasa *angalia, eleza, enda, gusa, hisi, inama, jenga, kaa, kata, kula, lala, lia, lima, ng'oa, ondoa, panda, piga, pika, safisha, sema, tafuta, toa, ua* na *weka* zilizo na hiponimu mbalimbali. Baadhi ya hiponimu za vitenzi hipanimu hizi ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| **Angalia** | : | angaanga, angalilia, chungulia, linga, ona, ota, perepesa. |
| **Eleza** | : | fafanua, fahamisha, gusia, lalamika. |
| **Enda** | : | andama, bingiria, chanyatia, chirizika, chopea, chuchia, churura, dema, duru, enda kijeshi, enda joshi, guchia, hangaika, hemera, iliya, kimbia, kokona, kweta, nengua, ogelea, ondoka, ongozana, paa, parakasa, randa, rombeza, ruka, sukuma, tambaa, tataga, tembea, tinga, tokomea, vuta. |

## Hitimisho

Makala haya yameonyesha kuwa hiponimia huweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia mikabala miwili ya kisayansi au ya kiisimu. Mkabala wa kisayansi hutumiwa kwa kuzingatia mifumo faafu inayorejelea sifa bainifu za kibiolojia. Mkabala huu aghalabu huangazia hiponimia za kategoria ya leksimu nomino inayohusiana tu na hipanimu *kiumbe hai*. Hivyo basi, hauwezi kutumiwa katika uchanganuzi wa hiponimia zinazorejelea nomino za vifaa, hali au hata matendo. Mkabala huu wa kisayansi huonyesha mgawanyo wa vijenzi vya hipanimu kwa kutumia mfumo wa taksonimia kamilifu au kisayansi. Mgawanyo unaodhihirika miongoni wa hiponimu tunapotumia mkabala huu huwa wa kudumu katika tafiti zote za wanasayansi. Hii inamaanisha kwamba, kila mtafiti anaporejelea kwa mfano hipanimu *kiumbe hai* kote ulimwenguni basi bila shaka atapata moja kwa moja *mmea* na *mnyama* kama hiponimu zake.

Mkabala wa kiisimu aghalabu hutumiwa na wanaisimu wengi na hurejelea hali ambapo hipanimu na hiponimu husika huchanganuliwa kwa mujibu wa mwelekeo au ubinafsi wa mwanaisimu pamoja na fasili zinazotolewa katika makala maalum ya leksikografia ya lugha husika. Kinachobainika katika mkabala huu wa kiisimu ni kwamba mwanaisimu yeyote ana uhuru wa kutoa na kuteua mifano ya hiponimu za hipanimu husika akizingatia njia zake tofautitofauti mradi tu madhumuni ya utafiti wake yametoshelezwa. Kutokana na uhuru kama huu, wanaisimu tofauti huweza kujitokeza na hiponimu tofauti tofauti hata kuhusu hipanimu moja maalum. Kama vile, hipanimu *mnyama* huweza kuwa na hiponimu kama vile *punda, ng'ombe* au *farasi* au kwa upande mwingine kuwa na *ng'amia, kondoo* na *sungura* mradi tu mtafiti ametaja mifano ya mnyama.

Imebainika vilevile katika makala hii kuwa uainishaji wa hiponimia za laksimu hasa za nomino na vitenzi hazipaswi kutolewa bila vigezo maalum. Hivyo basi, kuna vigezo mbalimbali vinavyorejelewa kama miainisho kuu inayoweza kutumiwa kufafanua hiponimia. Kama vile, uainishaji kitambuzi, kiuamilifu, kijiografia, kitukio, kihali na kitendo. Hiponimia mbalimbali za nomino hujumuishwa katika miainisho mitano ya kwanza hasa kitambuzi, kiuamilifu, kijiografia, kitukio na kihali. Hata hivyo, muainisho wa hiponimia kitendo hutumiwa kuainisha hiponimia za vitenzi. Aidha, mwanaisimu anahitajika kutumia vielelezo panapofaa ili kuonyesha namna hiponimia husika inavyojitokeza na kuwasilishwa katika matini kitaksonimia ama kamilifu au isiyo kamilifu.

## Marejeleo


Barker, C. (2001). *Lexical semantics.Encyclopedia of cognitive science*. San Diego USA: Macmillan References Ltd. Kutoka http://semanticsarchive.net/barker/Research/barker-lexical.pdf

Carter, R., & McCarthy, M. (1988). *Vocabulary and language teaching*. London: Longman.

Channell, J. (1994). *Vague language.* Oxford: Oxford University Press.

Cruse, D. A. (1986). *Lexical semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cruse, A. (2011). *Meaning in language: An introduction to semantics and pragmatics* (3rd ed.). Oxford: Oxford University Press.

Crystal, D. (1987). *Child language learning and linguistics: An overview for the teaching and therapeutic professions.* London: Edward Arnold.

Fromkin, V., Rodman, R., & Hyams, N. (2007). *An introduction to language*. Boston: Thomson Wadsworth.

Gao, C., & Xu, B. (2013). The application of semantic and field theory to English vocabulary learning. *Theory and Practice in Language Studies*, 3 (11), 2030-2035. Doi: 10.4304/tpls.3.11.2030-2035

Gibbe, A. G. (1977). *Homonymy, synonymy and antonymy in Kiswahili: A lexical study*. Tasnifu ya Uzamili. Dar es Salaam: Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.

Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Hatch, E., & Brown, C. (1995). *Vocabulary, semantics and language education.* Cambridge: Cambridge University Press.

Hoplant (2002). *The plant kingdom*. Kutoka http://www.botanicgardens.ie/educ/hoplant.pdf

Hornby, A. S. (Mh.) (2010). *Oxford Advanced Learner's Dictionary* (8thed.). Oxford: Oxford University Press.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya isimujamii*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Lyons, J. (1968). *Introduction to theoretical linguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1981). *Language and linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mdee, J. S., Njogu, K., & Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn.

Miller, A. G. (1991). *The science of words*. New York: Scientific American Library.

Murphy, M. L. (2003). *Semantic relations and their lexicon*. Cambridge University: Cambridge University Press. Kutoka www.sussex.ac.Uk/Users/lunnem/studies_in_informatics.pdf

Obuchi, S. M., & Mukhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na vipengele*. Nairobi: A~Frame Publishers.

Odoyo, B. O. (2006). *Uchanganuzi wa kileksika wa hiponimia katika Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

Okal B. O., Indede, F. & Mohochi, E. S. (2016). Uchanganuzi wa hiponimia za vitenzi vya Kiswahili. *Swahili Forum* (SF), vol. 23, 122-136, ISSN 1614-2373 (Online). Germany, Leipzig: Leipzig University.

Omogo, B. S. (1996). *Dhima ya ushikamano katika utendaji kwenye insha za Kiswahili za wanafunzi wa kidato cha nne wilayani Kisii Kenya.* Tasnifu ya Uzamili. Eldoret: Chuo Kikuu Cha Moi.

Rei, M., & Briscoe, T. (2014). Looking for hyponymy in vector space. *Proceedings of the Eighteenth Conference on Computational Language Learning, 68-77.* Kutoka www.ac/web.org/.../w14-1608

Roitman, J. (2011). *Introduction to set theory*. Kutoka www.math.ku.edu/~roitman/Stb3fullWeb.pdf

Stephan, F. (2009). *Set theory*. Kutoka www.compo.nus.edu.sg/~fstephan/settheory.pdf

TUKI (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. *Toleo la 3*. Nairobi: University of Dar es Salaam and Oxford University Press.

Westmoreland, & Esparza, K. (2005). *Phyla of the Animal Kingdom*. Kutoka http://www.art.com/asp/sp-asp/_/ui--9F63025C7D9144F79D1199082B3E4112/PD--10054920/sOrig--CAT/sOrigID--7444/Yosemite_Valley.htm#

Wierzbicka, A. (1988). *The semantics of grammar.* Amsterdam: John Benjamin's Publishing Co.

Yildirim, S., & Yildiz, T. (2012).Corpus driven hyponymy acquisition for Turkish language. Katika A. Gelbukh (mh), *CICLing 2012, Part I, LNCS 7181*, 29-41. Kutoka www.link.springer.com/chapter/10.1007/978-3-642-28604-9_3

Yule, G. (1996). *The study of language* (2nd ed.). Cambridge: Cambridge University Press.